# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANA
# OFISI YA RAIS,
# TAWALA ZA MIKOA ZA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA MANISPAA KAHAMA

**Kumb.Na KMC/L.40/8/133** **14 Mei, 2025**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Manispaa Kahama imepata idhini ya utekelezaji wa kibali cha Ajira Mpya katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa barua yenye Kumb. Na. FA.97/288/01/A/25 ya Tarehe 29 Aprili, 2025 kutoka kwa Katibu Mkuu ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Hivyo, Mkurugenzi wa Manispaa Kahama anawatangazia Watanzania wenye Sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa Kahama, kuomba nafasi hizo kuanzia tarehe 14 Mei, 2025

**1.0 Msaidizi wa Kumbukumbu II- NAFASI (04)**

**1.0.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Awe Na Elimu ya Kidato Cha Nne Au Kidato Cha Sita Mwenye Stashahada NTA level 6 katika Fani zifuatazo:

Utunzaji Wa Kumbukumbu, Urasimu Ramani (Catography) Au Geo-Informatics, Sheria, Au Kumbukumbu Za Afya Kutoka Vyuo Vinavyotambuliwa Na Serikali Na Mwenye Ujuzi Wa Kompyuta

**1.0.2 KAZI NA MAJUKUMU YA MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II**

I. Kuorodhesha barua zinazoingia masjala kwenye rejista (Incoming Correspondence Register)

Ii. Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya Taasisi (Outgoing Correspondence Register)

Iii. Kusambaza majalada kwa watendaji (Action Officers)

Iv. Kupokea majalada yanayorudi masjala kutoka kwa watendaji

V. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/majalada yanayohitajika na watendaji

Vi. Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (racks/filing cabinets) au mahali pengine yanapohifadhiwa

Vii. Kufuatilia mzunguko wa majalada ya taasisi (file tracking)

### 1.0.3 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya Serikali Ya **TGS C1** kwa mwezi

### 1.0.4 Dereva II- NAFASI (03)

#### SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na Elimu ya kidato cha Nne (IV) au kidato cha Sita (VI) na awe na ufaulu wa daraja la nne na kuendelea, awe mwadilifu na ambaye hajawahi kukutwa na hatia Mahakamani, awe amehudhuria mafunzo ya Msingi ya uendeshaji Magari ( Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au NIT au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali na Awe na leseni ya daraja C Au E.

### 1.0.5 KAZI NA MAJUKUMU YA DEREVA II

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
iii. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
iv. Kujaza na kutunza taarifa za safari katika daftari la safari
v. Kufanya usafi wa gari.

### 1.0.6 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya Serikali ya **TGS B1** kwa mwezi.

### 1.0.7 MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye ana umri wa miaka 18 mpaka 45
ii. Mwombaji aambatishe nakala ya Cheti cha kuzaliwa.
iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za Simu.
iv. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Elimu na taaluma kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, na vilivyothibitishwa na Wakili au Kamishna wa Viapo.
v. Testimonials, provision results, statement of results, havitakubaliwa
vi. Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE.
vii. Waomabji waambatanishe picha moja passport size ya hivi karibuni
viii. Barua ya Maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kingereza.

ix. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 27 Mei, 2025.

x. ***MUHIMU:*** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti, aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

Mkurugenzi wa Manispaa,
Barabara ya Boma,
S.L.P 472,
**KAHAMA – Shinyanga.**

xi. Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye Mfumo wa Kieletroniki wa Ajira ***(Recruitment Portal)*** kupitia anuani ifuatayo: https://portal.ajira.go.tz/ anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Secretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa **"Recruitment Portal"**

xii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Imetolewa na;

**MKURUGENZI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA**
**KAHAMA**

MUNICIPAL DIRECTOR
KAHAMA MUNICIPAL COUNCIL
P.O. Box 472
KAHAMA